

Haki zako na Wajibu

Hati ya Wateja wa Australia ya Kusini ya Mpango
wa Afya ya Umma



Government
of South Australia

SA Health

Maktaba ya Taifa ya Australia Kuingia katika Machapisho mbalimbali
Kichwa cha Habari: Haki na wajibu wako: katiba hiyo kwa wagonjwa wa mfumo wa afya ya
umma katika Australia ya Kusini / Serikali ya Australia ya Kusini, SA Health.

ISBN: 9780730898276 (pbk.)

Masomo: Sheria za Madawa na sheria - Australia ya Kusini
Mfanyakazi wa Afya na mgonjwa - Australia ya Kusini
Wagojwa wa Hospitali - Hali ya Kisheria, sheria, nk - Australia ya Kusini
Mgonjwa - hali ya Kisheria, sheria, nk - Australia ya Kusini.

Wandishi wengine/Waliochangia: South Australia. Dept. for Health and Ageing.

Dewey Number: 610.696

Haki Zako na Wajibu

SA Health ina nia ya kuhakikisha kwamba huduma za afya unazopokea ni salama, nzuri, ufanisi na zinazoheshimu haki yako kama mtu binafsi.

Upatikanaji

una haki ya kupata huduma za afya na huduma za jamii

Usalama

una haki ya kuwa salama kutokana na unyanyasaji

Ubora

una haki ya huduma bora za juu

Usalama

una haki ya kuchukuliwa kwa heshma

Habari

una haki ya kupewa taarifa

Kuhusika

una haki ya kushiriki kikamilifu

Usiri

una haki ya faragha na usiri

Maoni

una haki ya kutoa maoni na/ au kulalamika

The National Relay Service can provide assistance for people who require hearing and speaking assistance. National Relay Service: <http://relayservice.gov.au/> Phone: 1800 555 660. If you or your carer need help talking to the health professionals who are responsible for your care you can ask a staff member to arrange an interpreter for you free of charge. This book has been translated and is available on the SA Health website www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Amharic

የኢትዮጵያ የቃዬበላሽ አገልግሎት (The National Relay Service) የመስማትና የመኖር ድጋፍ ለሚሸራው ስምምነት ለሰጥ ይችላል፡፡ የዚህንም የቃዬበላሽ አገልግሎት (National Relay Service): <http://relayservice.gov.au/> የክልሉ ቁጥር: 1800 555 660 እርስዎ ወይም ተከተለበትም ለእርስዎ እንከተከበ ህሳኔ ተተቀብለትን የጊዜ በለመጀምሮች ለመስማት እርዳታ ከፈላጊ ተቀብለ የሚገባውን አስተርጓዣ እንዲያዘግዧው መጠየቅ ይችላል፡፡ ይህ መጽሐፍ ተተርጓዣል፡፡ በደቡብ አውጥቶች የጊዜ የጊዜ ላይ የተተካል www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Arabic

توفر خدمة البث الوطنية (National Relay Service) المساعدة للأشخاص الذين بحاجة للمساعدة في السمع والنطق. خدمة البث الوطني: <http://relayservice.gov.au/> هاتف: 1800 555 660 إذا كنت أنت أو من يرعاك بحاجة للمساعدة في التحدث مع مهنيي الصحة المسؤولين عن رعايتك، فإن إماكانتك الطالب من أحد الموظفين الترتيب لجيء مترجم مجاناً. تمت ترجمة هذا الكتيب وهو متاح على موقع دائرة صحة جنوب استراليا (SA Health) www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Chinese simplified

全国传递服务为有听障与语障的人士提供协助。全国传递服务的网址: <http://relayservice.gov.au/> 电话:1800 555 660 如果您或者您的照顾者需要同主治医生交流，但又不会讲英语，您可以要求一名工作人员为您安排一位传译员，此服务免费。本手册已译成多种语言，可以在SA Health的网站上获取: www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Chinese traditional

全國中繼服務可為需要聽力和語言協助的人提供幫助。全國中繼服務網址:<http://relayservice.gov.au/> 電話:1800 555 660 在與為您提供治療的專業醫護人員交流時，如果您或者您的看護者需要語言溝通方面的協助，可向有關工作人員要求安排傳譯員。此服務是免費的。本手冊已被譯成中文，可從南澳健康部網站獲得 www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Dari

خدمات رله ملي، افرادي که خصروت به کمکهای شنوایی و گفتاری دارند را کمک کرده می تواند. خدمات رله می: /<http://relayservice.gov.au/> تلفون: 1800 555 660 اگر شما یا مراقب شما برای صحبت با کارکنان مسلکی خدمات صحی که مسولیت مراقبت از شما را بر عهده دارند احتیاج به کمک دارید از یکی از کارکنان بخواهید تا بطور مجاني برای شما ترجمان بگیرد. این جزوی به زبانهای مختلف ترجمه شده و در وب سایت SA Health در www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities در دسترس می باشد.

Dinka

Aguir Baai Wël Cuot a lëu bë kœc kony të ye kek kœc wic kuɔɔny ë piipjir ku jam.
Aguir Baai Wël Cuot: <http://relayservice.gov.au/> Telepun: 1800 555 660. Na wic dumuök du kuɔɔny bë jam kek kœc panakim wén kek gém yi döc, ka yin a lëu ba jam kek kœc panakim bik yi wiēc raan bï waar thok ku kën a bik looi majan. Athör kën a cë waar yic thok kök ku a tbü lɔkayukar ë Pial Guöp SA tën www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Greek

Η Εθνική Υπηρεσία Αναμετάδοσης δύναται να παράσχει βοήθεια σε άτομα που χρειάζονται βοήθεια ακοής και ομιλίας. Εθνική Υπηρεσία Αναμετάδοσης (National Relay Service):

<http://relayservice.gov.au/> Τηλέφωνο: 1800 555 660. Αν εσείς ή φροντιστής σας χρειάζεστε βοήθεια για να μιλήσετε στους επαγγελματίες υγείας οι οποίοι είναι υπεύθυνοι για τη φροντίδα σας μπορείτε να ζητήσετε από ένα μέλος του προσωπικού να διευθετήσει δωρεάν διερμηνέα για σας. Το βιβλιάριο αυτό έχει μεταφρασθεί και διατίθεται στην ιστοσελίδα SA Health www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Italian

L'ufficio National Relay Service può fornire assistenza a persone che necessitano di aiuto per udire e parlare. National Relay Service: <http://relayservice.gov.au/> Telefono: 1800 555 660.

Se voi o il vostro badante avete bisogno di aiuto per parlare con lo staff medico che vi assiste potete chiedere ad un impiegato del nostro personale di chiamare un interprete gratuitamente. Questo libretto è stato tradotto ed è disponibile sul sito web SA Health www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Khmer

សេវា National Relay Service អាចផ្តល់ជូនដំឡើយសម្រាប់អ្នកដើរត្រូវការដំឡើយភ្លាស់ប៉ុណ្ណោះ និងនិយាយ។ សេវា <http://relayservice.gov.au/> ទូរស័ព្ទ: 1800 555 660 បច្ចុនបៀអ្នក បុង្ហាញកំបែទៅបែសអ្នកត្រូវការដំឡើយភ្លាស់ប៉ុណ្ណោះ ទៅការអ្នកដែលនៅថ្ងៃក្នុងសុខភាពដែលទទួលខុសត្រូវប៉ុណ្ណោះ ការដំឡើយភ្លាស់ប៉ុណ្ណោះ ហើយអ្នកអាចស្វែងសុំសមាជិកបុគ្គលិកក្នុងរៀបចំអ្នកប៉ុណ្ណោះ ដែលអ្នកដោយតាមតិចតាមទំនួន។ សៀវភៅនេះបានបង្កើតឡើងដោយ SA Health: www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Russian

Национальная релейная служба может оказать помощь людям, которые имеют нарушения слуха или речи. Национальная релейная служба: <http://relayservice.gov.au/> Телефон: 1800 555 660. Если вам или лицу, осуществляющему за вами уход, необходима помощь во время беседы с медицинскими работниками, которые отвечают за предоставление для вас услуг по здравоохранению, вы можете попросить сотрудника, чтобы вам бесплатно предоставили переводчика. Эта книга была переведена и доступна на веб-сайте SA Health www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Spanish

El Servicio de Transmisión Nacional brinda apoyo a las personas que necesitan ayuda debido a problemas de audición o del habla. Servicio de Transmisión Nacional: <http://relayservice.gov.au/> Teléfono: 1800 555 660. Si usted o su cuidador necesitan ayuda para hablar con los profesionales de salud que están a cargo de su cuidado, puede pedirle a un miembro del personal que organice un intérprete de manera gratuita. Este folleto ha sido traducido y está a su disposición en la página web de SA Health www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Somali

Adeega Baahinta Quranka ayaa taageero siin kara dadka in laga caawiyo u baahan hadalka iyo maqalkaba. AdeeggaBaahinta Quranka: <http://relayservice.gov.au/> / Telefoon: 1800 555 660. Haddi adiga iyo daryeelahaaga aad u baahataan in leydiinka kaalmeeyo la hadalka xirfadlayasha caafimaadka ee masuulka ka ah daryelkaaga waxaad weddiin kartaa mid ka mid ah shaqaalahaa in uu kuu diyaariyo turjubaan bilaash ah. Buuga ayaa la tarjumay waxaana laga helaa website ka Hay'adda Caafimaadka Koofurta Awstaraaliya: www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Swahili

Huduma ya Kuunganisha ya Taifa inaweza kutoa msaada kwa watu wanaohitaji msaada wa kusikia na kuongea. Huduma ya Kuunganisha ya Taifa: <http://relayservice.gov.au/> Simu: 1800 555 660. Kama wewe au mlezi wako anahitaji msaada wa kuzungumza na wataalamu wa afya ambao wanawajibika kwa huduma yako unaweza kuiliza mfanyikazi kupanga mkalimani kwa ajili yako bila malipo. Kitabu hiki kimetafsiriwa na kinapatikana kwenye tovuti ya SA Health. www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Tagalog

Ang Pambansang Serbisyo ng Paghahatid ay nagbibigay ng tulong sa mga taong mahina ang pandinig at hirap sa pagsasalita. Pambansang Serbisyo ng Paghahatid: <http://relayservice.gov.au/> Telefono: 1800 555 660. Kung ikaw o ang iyong tagapag-alaga ay kailangan ng tulong sa pakikipag-usap sa mga propesyonal na may pananagutan sa iyong pangangalaga, maari kang makipag-usap sa isang kawani upang mabigyan ka nang interprete na walang bayad. Ang aklat na ito ay isinalin at makukuha sa websayt ng Kalusugan SA: www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities

Tamil

செவி மடுப்பு மற்றும் பேச்சு விடயங்களில் உதவி தேவைப்பூபவர்களுக்கு ‘நேஷனல் ரிலே செவிஸ்’ – இனால் உதவ இயலும். ‘நேஷனல் ரிலே செவிஸ்’: <http://relayservice.gov.au/> தொலைபேரி: 1800 555 660. உங்களுடைய கவனிப்பிற்குப் பொறுப்பாக இருக்கும் சுகாதார் தொழிலர்களுடன் பேசுவதில் உங்களுக்கோ அல்லது உங்களுடைய கவனிப்பாளருக்கோ உதவி தேவைப்பட்டால், இலாபமாக வெளியீர்த்துறைப்பாளர் ஒருவரை ஏற்றாடு செய்து தருமாறு எமது ஜூபியர் நின்கள் கேட்கலாம். இந்த நிலை மொழியீர்க்கப்பட்டுள்ளது, மற்றும் www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities எனும் ‘SA சுகாதார்’ வலைத்தவற்றில் இது கிடைக்கும்.

Vietnamese

Dịch Vụ Tiếp Âm Quốc Gia (The National Relay Service) có thể cung cấp các dịch vụ hỗ trợ những người cần trợ giúp trong việc nghe và nói. Dịch Vụ Tiếp Âm Quốc Gia (National Relay Service): <http://relayservice.gov.au/> Điện thoại: 1800 555 660. Nếu quý vị hoặc người chăm sóc quý vị cần trợ giúp để nói chuyện với nhân viên y tế đang chịu trách nhiệm về sức khỏe của quý vị, quý vị có thể yêu cầu thu xếp một người thông ngôn miễn phí. Quyền sách này đã được dịch và có thể tìm thấy trên trang web của Bộ Y Tế Nam Úc www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities



Kituo cha Utafsiri na Ukalimani wa
Lugha Kupiga Bure: 1800 280 203
<https://www.translate.sa.gov.au/>

Yaliyomo

Kujiaminisha kwa matunzo na huduma	7
Matunzo ya afya yako – jinsi unanyoweza kusaidia	9
1. Upatikanaji – haki ya kupata huduma za afya na jamii	10
Upasuaji wa Kuchaguliwa na listi ya kusubiri	10
Timu ya Afya wa Aborigino	11
2. Usalama – haki ya kuwa salama kutokana na unyanyasaji	11
3. Ubora – haki ya huduma bora za juu	12
4. Heshima – haki ya kutendewa kwa heshima	13
Mielekeo ya Huduma ya Juu	13
5. Habari – haki ya kupewa taarifa	14
Hospitali za wagojwa binafsi au za kujitegemea	15
Msaada wa gharama na kifedha	15
Huduma za SA Ambulance	17
Mpango wa Msaada wa Usafiri wa Wagojwa (PATS)	17
6. Kuhusika – haki ya kuhusika ipasavyo	18
Ruhusa	19
Wanafunzi	19
Watumiaji wa Afya ya Akili	19
Wafanyakazi wazoefu wanaoishi katika huduma ya afya ya akili	20
Watoto	20
7. Usiri – haki ya faragha na usiri	21
Ni lini habari zako binafsi zinaweza kuchangiwa	21
Kutumia habari ili kuboresha huduma za afya	22
8. Maoni – haki ya kutoa maoni na/au malalamiko	23
Rufaa	25

Kujiaminisha kwa matunzo na huduma

SA Health ina nia ya kutoa uzoefu mzuri kwa watu wote wanaopata huduma ya afya na jamii. Ili kufanikisha hili tunataka kutoa huduma ambazo hukuza huduma zinazojali mtu.

Tunataka kutoa huduma ambazo ni salama, zilizoratibiwa na kuheshimu haki zako na hesima.

Kama wewe, familia yako au walezi mna maswali yoyote au wasiwasi au wanahitaji msaada wa kuelewa kilichosemwa ili uweza kufanya maamuzi sahihi, tafadhalii uliza mtu yeyote wa timu ya huduma ya afya yako. Wafanyakazi wanaweza kupanga mkalimani kwa ajili yenu kama inahitajika.



Malalamiko ya Mkataba wa Kamishna wa Huduma ya Afya za Jamii wa Haki za Afya na Huduma za Jamii zinapatikana pia katika www.hcsc.sa.gov.au. Mkataba unaonyesha haki zako, na wale wa familia yako, walezi au watu ambao umewachagua kuhusika kwa niaba yako. Sisi tunatafuta kuboresha huduma zetu kwa kuhakikisha kuwa haki zako zinashughulikiwa ipasavyo .

SA Health imetengeneza maelezo manne maalum ya vipeperushi vya Haki kwa ajili ya wagonjwa wa afya ya akili, walezi na familia. Hizi zinapatikana kwenye www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities.

SA Health pia ina maadili na nia ya::

- > Jukumu la walezi, ikiwa ni pamoja walezi vijana, ndani ya huduma zetu za afya. Tazama mwongozo wa Australia ya Kusini wa Walezi na habari zaidi juu ya haki za walezi ndani ya mfumo wa afya www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities
- > The Kauli ya Taifa ya Afya ya Akili ya Haki na Majukumu www.health.gov.au kisha tafuta Kauli ya Taifa ya Afya ya Akili ya Haki na Majukumu
- > Mkakati wa Kulinda Haki za Wazee wa Australia ya Kusini www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities
- > Mkataba wa Haki kwa Watoto na Vijana katika Matunzo www.gcyp.sa.gov.au/charter-of-rights-2/the-charter/
- > Haki za Watoto na Vijana katika Huduma za Afya <https://children.wcha.asn.au/children-and-young-peoples-rightshealthcareservices-charter>

Matunzo ya afya yako – jinsi unanyoweza kusaidia

Huduma nzuri za afya zinafikiwa kwa kushirikiana kati ya wewe na wataalamu wa afya wa huduma yako. Ili kutusaidia kutoa huduma bora kwako i muhimu wewe:

- > Mwambie wafanyakazi kama unahitaji mælezo zaidi au kama kuna jambo lolote ambalo hauelewi au una wasiwasi nalo.
- > Fuata mpango wako wa afya au mwambie mtaalamu wa afya kama wewe hataki au huwezi kufanya hivyo.

Habari ambazo unatakiwa kuwambia wafanyakazi wa afya:

- > Historia yako ya matibabu na ya familia yako. Hii ni pamoja na matatizo yoyote, matatizo au athari mbaya ambazo ulizipitia.
- > Matibabu yoyote au dawa yoyote ambayo (au lazima) unatumia ikiwa ni pamoja na kutimiza, asilia au dawa mbadala yoyote.
- > Mabadiliko ya hali yako, ikiwa ni pamoja na matatizo yoyote unayoweza kuwa nayo na dawa yoyote au matibabu uliyoyapokea.
- > Mahitaji maalum yoyoye uliyonayo, ikiwa ni pamoja na yale ya umuhimu kiutamaduni au kidini au kama matokeo ya ulemavu.

Tafadhali jali watumishi na wagonjwa wengine:

- > Vitendo vya vurugu, kuapishwa, vitisho au kuwatukana wagonjwa wengine, ndugu au mtumishi haikubaliki.
- > Tekeleza miadi yako. Kama huwezi kutimiza miadi tafadhali julisha huduma ya afya haraka iwezekanavyo ili kuwezesha miadi ibadilishwe tarehe.
- > Fahamu mahitaji ya wagonjwa wengine na faragha zao.
- > Usilete pombe, vitu haramu au silaha kwa huduma yoyote ya afya.
- > Eneo la huduma za hospitali na afya haliruhusiwi kuvutiwa sigara.

Haki za Mkataba wa Afya na Huduma za Jamii

1. Upatikanaji – haki ya kupata huduma za afya na jamii

Wana Australia wa Kusini wote wana haki ya kupata huduma za afya na jamii ambazo zinakidhi mahitaji yao.

Huduma za afya hutolewa kwa watu wote kwa zingatia tathmini ya hali yako wa uharaka wa matibabu unahitaji.

SA Health ina mipango iliyopo ili kusaidia makundi ya watu ambaa wanaweza kukabiliwa na ugumu katika kupata huduma. Kwa mfano, watu wenye mahitaji ya afya ya akili, watu wenye ulemavu, watu wenye vikwazo vya lugha na kisomo, kusema au mataitizo ya kusikia, watu wenye tofauti ya imani za kitamaduni, na watu ambaa ni dhaifu kabisa. Kama unahitaji msaada wa kupata huduma, tafadhali kujadiliana hili na wafanyakazi kutoka huduma ya afya yako.

Upasuaji wa Kuchaguliwa na listi ya kusubiri

Kama hali yako si kutishia maisha, unaweza kuwekwa kwenye orodha ya wanaosubiria matibabu/upasuaji. Baadhi afya za jamii na huduma za afya za meno pia wana utaratibu wa orodha ya kusubiri. Taarifa kuhusu orodha ya kusubiri inaweza kupatikana kwenye ubao wa kuchaguliwa wa upasuaji katika www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities.

Una haki:

- > kujua wakati wako wa kusubiria
- > kujua kama kuna huduma nyingine za afya ambapo kusubiri kunaweza kuwa kufupi, au kama kuna chaguzi nyingine kwa ajili ya matibabu ya awali au mbadala.

Kama hali yako ikiwa mbaya zaidi, jadili hili na Daktari wako wa Familia (GP).

Timu za Afya za Aborigino

Baadhi ya hospitali na huduma za afya zina Timu za Afya za Aborigino. Unaweza kuuliza wafanyakazi kama Timu ya Afya ya Aborigino au Afisa wa Afya wa Ushirikiano wa Aborigino anapatikana.

Wanaweza kukusaidia na maelezo ya jinsi hospitali inavyofanya kazi, kinachoendelea, na kukupa taarifa kuhusu kupanga usafiri au malazi.

Ukitoka hospitali wanaweza kukuunbganisha na wafanyakazi wa huduma za afya ya jamii za Aborigino na Torres Strait Islander na Huduma za Afya za Jumuia ya Aborigino, kutegemea na nini unahitaji.

Timu ya Afya ya Aborigino ina lengo la kusaidia watumiaji wote wa huduma za Aborigino ambao wanahitaji msaada, hata hivyo kuna kipaumbele cha juu kwa watu wa asili na Torres Strait Islander kutoka maeneo ya vijijini na kijijini.

2. Usalama – haki ya kuwa salama kutokana na unyanyasaji

SA Health inatambua kuwa wagonjwa/wateja, walezi, wakujitolea na wafanyakazi wote wanataka huduma ya afya ambayo inaweza kutolewa na kupokelewa bila ya tishio binafsi au hatari.

Hospitali na huduma za afya ni maeneo ya uponyaji na huduma. Tutafanya kila linalowezekana ili kuwalinda vizuri na salama na kutoa huduma ambayo inatolewa kwa huruma, upendo na kupunguza dhiki:

- > una haki ya kuwa salama kutokana na madhara na unyanyasaji
- > una haki ya kupata huduma zinazotolewa kwa masharti madogo
- > una haki ya kupata huduma ambayo itapunguza ajari au madhara yasiyotarajiwa

Hospitali na huduma za afya pia ni maeneo ya kazi.

Tafadhali jaribu kujali watumishi, wagonjwa wengine na wageni. Tabia ambayo inatishia usalama wa wafanyakazi au wagonjwa wengine, kama vile matusi ya mdomo au kimwili hayakubaliki.

Watu ambao wana tabia za kukera au namna ya hatari, wanaweza kuombwa kuondoka, au polisi au usalama wanaweza kuitwa.

Tafadhali chunguza dalili zozote za onyo na kusimamia watoto wakati wote.

Wafanyakazi ambao hutoa huduma na wewe nyumbani na wana haki ya kufanya kazi katika mazingira salama ya kazi. Kabla ya kutembelea wewe nyumbani, wafanyakazi watakupigia na kuangalia usalama.

3. Ubora – haki ya huduma bora za juu

SA Health ina nia ya kuhakikisha Australia ya Kusini ina mfumo wa huduma za afya zilizo salama, kuaminika na ubora wa juu.

Tunafanya hivyo kwa kuwa sera, taratibu na mazoea katika sehemu inayofuata kanuni za kisheria, kitaalamu, kimaadili, usalama na viwango vya ubora wetu.

SA Health imeendelea kufanya mapitio ya njia mambo yanayofanyika ili kuhakikisha usalama na huduma bora ya juu. Tuna wafanyakazi wenyewe elimu ya kutosha na vifaa ili kutoa huduma bora za afya. Unaweza kutarajia kwamba huduma zetu za afya zitashirikiana na huduma yako itaratibiwa ili kukidhi mahitaji yako.

Karatasi ya ukweli 'Karatasi ya Ukweli ya Kutembelea daktari wako - Matokeo zaidi ya ziara yako na daktari au mtoaji wa afya yako' inapatikana kwa: www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities.

4. Heshima – haki ya kutendewa kwa heshima

Una haki ya kutibiwa kwa heshima, hadhi na heshima bila kujali umri, jinsia, dini au utamaduni.

Una haki ya kuwa na matakwa yako, imani na matendo kuweza kuheshimiwa na kuonekana katika mpango kwa ajili ya huduma ya afya yako. Wafanyakazi wataheshimu utu wako.

Una haki ya kuweka kumbukumbu matakwa yako mapema kwa ajili ya matibabu na huduma za afya na kwa maamuzi yako ya kuheshimiwa na wale wanaojali kwa ajili yako.

Matakwa yako yanaweza kuhifadhiwa kupitia sheria ya Mwelekeo wa Huduma wa Juu au Mipango ya Matunzo ya Juu ya kawaida.

Mielekeo ya Huduma ya Juu

Mwelekeo wa Huduma wa Juu utawezesha kufanya mipango ya wazi ya kisheria kwa ajili ya huduma yako ya baadaye ya afya, mwisho wa maisha, mipango ya maisha unayoipendelea na mambo mengine binafsi juu ya fomu ya pekee ya Mwelekeo wa Huduma ya Juu.

Mwelekeo wa Huduma wa Juu hutumika katika kipindi chochote cha kushidwa ufanya maamuzi, ambayo yanaweza kuwa ya muda au ya kudumu.

Tafadhalii mwambie mfanyakazi wa huduma ya afya kama una Mwelekeo wa Huduma wa Juu na kutoa nakala ya hati ya timu ya hospitali ya kulazwa, na kwa daktari wako, na kwa Mwamuzi wako wa Mbadala.

Kwa habari zaidi na kupata Fomu ya Mwelekeo wa Afya wa Juu www.advancecaredirectives.sa.gov.au.

5. Habari – haki ya kupewa taarifa

Una haki ya kuanzisha, mawasiliano ya wazi na kwa wakati unaotakiwa kuhusu huduma, matibabu ya chaguzi na gharama katika njia ambayo unaweza kuielewa.

Kama mgonjwa, wewe au mwakilishi wa afya yako unaweza kutarajia¹:

- > kuwa na taarifa zote ulizopewa na wewe katika lugha/njia unaweza kuielewa
- > kuambiwa hatari yoyote ambayo wewe au mtu wa busara katika msimamo ulio sawa unaoweza kuzingatia kuwa muhimu, na hatari hizo kuweza kuelezewa kwako
- > kuambiwa ni matibabu yapi ambayo mtaalamu wako wa afya anapendekeza na njia zingine zozote mbadala ambazo ni sahihi ili uweze kufanya maamuzi sahihi kuhusu huduma ya afya yako
- > kupewa mælezo kuhusu vipimo, ikiwa ni pamoja na kuhusu hatari, na kuwa na matokeo na athari za matokeo hayo kuweza kuelezewa kwako
- > kujuua kusudi, faida na uwezekano wa madhara ya kutibu na/au dawa ulizopewa
- > kuweza kupewe mælezo ya nafasi ya mafanikio, haja ya matibabu mengine zaidi, uwezekano wa kurudia kwenye afya nzuri, kufufua na ukarabati
- > kuweza kupewe mælezo ya wazi ya kile kinachotokea kama mambo yakienda vibaya au si kama ulivyotarajiwa
- > kubadili akili yako, au kukataa mtihani au matibabu wakati wowote na kwa kujulishwa kuhusu matokeo ya kukataa vipimo au matibabu
- > kujuua kama tiba ni majaribio au zinatumika katika utafiti
- > kushaurishwa na kupewa mpango wa utekelezaji, kabla ya kutekeleza, ikiwa kama daktari wako wa kutibu ana maoni kuwa hali yako haihitaji kuendelea kukaa katika hospitali au huduma nyingine za afya

1 Mwakilishi ni Mtu Anayefanya Maamuzi wa kuchaguliwa, Mtu anayehusika au mzazi au mlezi wa mtoto.

- > kupewe habari kuhusu huduma za afya, vyama maalum, misaada, vifaa na huduma, ambayo vinaweza kukusaidia
- > kama daktari wako wa kukutibu ana maoni kuwa huduma sahihi zaidi inapatikana katika hospitali nyingine au kituo, na kwamba unaweza kuhamishiwa hiyo hospitali.

Hospitali za wagojwa binafsi au za kujitegemea

Wakati unahudhuria hospitali ya umma una haki ya kumchagua kuhudumiwa kama mgonjwa wa umma au binafsi bila kujali binafsi hali yako ya bima ya afya. Mfanyakazi atakuuliza kuchagua upendeleo wako kwa maandishi.

Una haki ya kujua uamuzi una maana gani na madhara ya kifedha ya uchaguzi wako

Kama mgonjwa wa umma huwezi kuchagua daktari wako mwenyewe na utatibiwa na daktari uliyepewa na hospitali. (Huduma baadhi za afya ikiwa ni pamoja na huduma za meno na idara ya dharura ya vijijini hufanya kuwa ada).

Mgojwa mwenye bima ya afya binafsi anaweza kuchagua kuweza kutibiwa kama mgonjwa wa umma.

Kama mgonjwa wa binafsi utatibiwa na daktari wako uliyemchangua, kitu mhimu tu ni daktari awe na mamlaka ya kufanya kutibu katika hospitali hiyo na anakubali kukutibu wewe kama mgonjwa wa binafsi katika hospitali hiyo. Wagonjwa binafsi wanawajibika kwa malipo ya ada zote.

Kama wewe haustahili kwa Medicare au kushiriki katika fidia ya madai mbadala ya mgonjwa kufanya uchaguzi hivyo mipango ya kulipa gharama itatumika.

Msaada wa gharama na kifedha

Wakazi wote wa Australia wenyе kadi ya Medicare wanastahili kutibiwa bure bila malipo kama mgonjwa wa umma katika hospitali za umma. Katika kesi nyingi, huduma zote katika mfumo wa afya ya umma katika Australia ya Kusini hutolewa bure bila malipo kwa wagonjwa umma. Kama utatakiwa kulipa ada yoyote utaambiwa mapema na kupewa akaunti.

Kama ukitibiwa kama mgojwa binafsi utatakiwa kulipa:

- > gharama za malazi ya hospitali
- > gharama za matibabu uchunguzi, prosthese na vifaa, misaada na vifaa vyahuduma za meno.

Gharama hizi zinaweza kulipiwa na mfuko wa bima yako ya binafsi ya afya yako, lakini unahitaji kujadili hili na bima yako kabla ya kulazwa hospitalini.

Aina mbalimbali ya mipango ya ada inatumika kwa wageni kutoka nje ya nchi au wamiliki wa visa ya mda. Unaweza kuangalia kustahiki kwako na Medicare kwenye simu 13 20 11 au pigia AusHealth: 1800 724 457 au barua pepe info@aushealth.com.au.

Huduma za SA Ambulance

Huduma ya SA Ambulance hutoa msaada wa matibabu ya dharura, matibabu na usafiri, usafiri kwa matukio yasiyo ya dharura na ubora wa huduma ya mgonjwa kwa watu wa Australia ya Kusini.

Unaweza kutakiwa kulipa ada kwa ajili ya huduma ya ambulance. Gharama ya Ambulance hailipwa na Medicare na huduma za ambulance haziwezi kukujulisha ada hii kabla ya kutoa usafiri.

Mfuko wa bima binafsi ya afya inaweza kufidia gharama ya gari la wagonjwa. Wasiliana na mfuko wa bima ya afya yako.

Kama unahitaji gari la wagonjwa wakati wewe umeruhusiwa kutoka hospitali utaulizwa uweze kufidia ada inayotakiwa.

Watu wanaowekwa chini ya amari isiyo ya halali ya matibabu au Sehemu ya 56 ya Sheria ya Afya 2009 inaweza kuwa kwamba ada zao huduma ya SA Ambulance zimelipiwa na Afya zao za Mahali.

Huduma ya SA Ambulance hutoa bima ya ambulance ya kusaidia na gharama. Kwa habari zaidi, habari zinapatikana kwenye www.saambulance.com.au au simu: 1300 13 62 72.

Kuwasiliana Huduma ya SA Ambulance katika tukio la dharura piga simu 000

Mpango wa Msaada wa Usafiri wa Wagojwa (PATS)

Mpango wa Msaada wa Usafiri wa Wagojwa (PATS) ni mpango wa ruzuku ambao hutoa fedha za kulipia baadhi ya usafiri, gharama za kusindikiza na malazi wakati watu wa Australia ya Kusini wanaoishi vijijini au porini wakisafiri zaidi ya kilomita 100 kuona wataalamu wa karibu. Kupokea ruzuku ya PATS unahitaji:

- > tazama na ofisi yako ya mahali ya PATS kuona kama unastahili kwa msaada
- > uliza ofisi ya mahali ya PATS ili kutuma fomu ya maombi au fungua fomu kutoka kwenye tovuti.

Habari na mawasiliano kutoka kwenye ofisi ya mahali ya PATS vinapatikana kwenye www.sahealth.sa.gov.au/PATS simu 08 8226 7215.

6. Kuhusika – haki ya kuhusika ipasavyo

Wakati wa kufanya maamuzi au kutoa idhini yako kuhusu utunzaji wako, vipimo na matibabu una haki ya:

- > kushirikishwa katika maamuzi yote juu ya huduma yako na kuuliza maswali ili kuelewa nini inaweza kutokea
 - > wapewe muda wa kufikiria na kujadili huduma yako ya afya na chaguzi za matibabu na familia yako, marafiki zao, walezi au maamuzi mbadala²
 - > kutafuta maoni ya pili na/au taarifa kuhusu utambuzi na matibabu yako ya chaguzi
 - > kupewa mælezo ya uwezekano wa matokeo ya kutopata ushauri wa kitaalamu wa afya
 - > kuteua mtu mwingine mbadala wa kufanya maamuzi kwa ajili yako wakati wewe hauwezi
 - > kuungwa mkono kufanya uamuzi kuhusu utunzaji wako au matibabu kama una uwezo wa kufanya uamuzi. Kama huna uwezo wa kufanya uamuzi, Mtoaji Maamuzi wako Mbadala au mtu anayehusika³ atapewa taarifa kuwasiliana kama watakuwa wanapatikana na wako tayari kufanya uamuzi kwa niaba yako
 - > kukataa matibabu ya muda mrefu na kupokea huduma tulivu na faraja badala yake
 - > kukataa kushiriki katika utafiti wa matibabu au majaribio
 - > kujitoa mwenyewe kutoka kwenye huduma za afya wakati wowote katika hatari yako mwenyewe isipokuwa kama uko chini ya amri ya jamii au matibabu chini ya Sheria ya Afya 2009 au unatakiwa kukaa hospitalini kwa matibabu kwa sababu uko juu ya amri ya kifungu cha 32 chini ya Ulezzi na Utawala wa sheria ya 1993 kutoka Mahakama ya Australia ya Kusini wa Jamii (zamani Bodi ya Ulezzi).
2. Mfanya Maamuzi Mbadala ni mtu au watu unaowaamini kufanya maamuzi kwa ajili yenu wakati wewe huwezi.
 3. Mtu anayewajibika ni mshiriki wa familia, rafiki wa karibu au mtu anayekubalika kiutamaduni kutoka kwa jamii hiyo.

Ruhusa

Unaweza kuulizwa kutia saini fomu ya idhini kudhibitisha umeidhinisha kuwa matibabu au vipimo kuwa vimeelezewa kwako. Ni wajibu wa mtaalamu wako wa afya kuamua kama wewe una uwezo wa kukubali matibabu, au huduma ya afya.

Katika hali fulani, matibabu ya dharura yanaweza kutolewa bila idhini yako, kama kuna tishio ya haraka kwa maisha yako au afya.

Hii inaweza kuwa kesi, isipokuwa kama awali zilionyesha kuwa wewe umekataa kuidhinisha matibabu au kuna mwakilishi anayepatikana, wakati huo, kwa kutoa idhini kwa niaba yako kwa matibabu ya dharura.

Wanafunzi

Wanafunzi wa Udaktari, uuguzi na washirika wa afya mara nyingi wanakuwepo au wanaweza kutoa matibabu chini ya usimamizi katika hospitali za umma na huduma za afya kwa idhini yako. Hii ni sehemu muhimu ya elimu yao.

Watumiaji wa Afya ya Akili

Una haki sawa kwa matibabu na huduma kama kila mtu mwingine.

Kama uko chini ya matibabu ya jamii au matibabu ya ndani chini ya Afya ya Akili ya 2009, unaweza kupewa matibabu bila idhini yako.

Matibabu lazima angalau yawe ya chaguo kwa kipindi cha muda mfupi unaostahili. Ni lazima iwe inayolenga kuleta uponyaji na kuzingatia matakwa yoyote ambayo umeyafanya kuititia Mwelekeo wa Malezi wa Juu au Mkataba wa Ulysses.⁴

Mfanya Maamuzi wako wa Mbadala au Mtu Anayewajibika wanaweza kufanya maamuzi kama wewe hauwezi.

4. Mkataba wa Ulysses ni mpango uliotengenezwa na familia na wataalamu wa afya ya akili kuhusu huduma ya watoto, kwa wakati wazazi wanapojsikia vibaya kama matokeo ya ugonjwa wa akili.

Wafanyakazi wazœfu wanaoishi katika huduma ya afya ya akili

Wafanyakazi wenye uzoefu wa kuishi ni watu ambao wamekuwa wagonjwa wa afya ya akili/walaji au walezi wao. Wafanyakazi wenye Uzoefu wa Kuishi wanapatikana katika vitengo vyote vya afya ya akili papo hapo na wanaweza kukusaidia, familia yako na marafiki kwa kutoa taarifa na msaada.

Watoto

Kama mzazi⁵ au mlezi wa mtoto, una haki ya kufanya maamuzi kwa niaba ya mtoto wako. Unaweza kukaa na mtoto wako katika hospitali na huduma yoyote ya afya, isipokuwa pale ambapo kujitenga ni muhimu kwa ajili ya dharura ya matibabu au sababu nyingine ya matibabu. Watoto pia wana haki ya kuwa na wazazi au walezi wao wa sasa.

Jinsi watoto wanavyokuwa wakubwa (zaidi ya umri wa miaka 16) wana haki ya kushauriwa na kufanya maamuzi kwa niaba yao wenyewe. Mtaalamu wa afya anaweza kutoa matibabu kwa mtoto chini ya miaka 16 kama mtoto akitoa ruhusa na mtaalamu wa matibabu ameridhika kwamba mtoto ana uwezo wa kuelewa matibabu, na mtaalamu mwengine wa afya anakubaliana na maoni hayo.

5 Hii ni pamoja na wazazi wa kambo au watu wazima badala ya wazazi wa mtoto ambayo ina maana kwamba mtu huyu ana wajibu wa majukumu ya wazazi siku kwa siku kwa mtoto, kwa mfano mababu hutunza watoto kwa niaba ya mzazi wa mtoto huyo.

7. Usiri – haki ya faragha na usiri

Usiri wako na haki ya usiri itaweza kuhestimiwa wakati wote

Habari kuhusu wewe zitakusanya na SA Health kutoa tiba na huduma.

Habari zako zinahifadhiwa kwa usalama na upatikanaji wa habari zako zinalidwa kwa wale wanaohusika katika huduma yako.

Unaweza kukataa kutoa taarifa, lakini hii inaweza kuwa na athari juu ya huduma yako au matibabu.

Una haki ya kuomba na kuweza kuona kumbukumbu yako ya afya, isipokuwa kama kuna kizuizi cha kisheria kilichowekwa.

Kama unaamini maelezo katika rekodi yako binafsi ya afya sio sahihi, imepita tarehe au kupotosha, unaweza kuomba rekodi kufanyiwa marekebisho.

Zungumza na wafanyakazi wa huduma za afya kuhusu jinsi ya kufanya hivyo.

Ni lini habari zako binafsi zinaweza kuchangiwa

Wataalamu wa afya wanaweza kutumia rekodi yako binafsi ya afya kwa kuwasiliana na wengine kuhusu huduma unayoipokea kupokea. Sheria ya Afya ya mwaka 2008 na Sheria ya Afya ya Akili ya 2009 inaonyesha ni wakati habari kuhusu wewe zinaweza kuwa wazi kwa watu wengine au watoa huduma.

Maelezo yako ya kibinafsi yanaweza kuwa pamoja na huduma nyingine za afya kupanga huduma kwa ajili yenu wakati ukiondoka hospitali.

Habari zako binafsi zinaweza kushirikishwa, kwa ruhusa yako:

> na bima yako mfuko wa afya au

> upande wa tatu kama vile Kinga ya Kazini au Kamishna ya Ajari ya Magari

Wakati mwingine SA Health inaweza kutakiwa au kuidhinishwa na sheria kutoa taarifa kuhusu wewe na wengine bila idhini yako. Hii ni pamoja na wakati ni muhimu ili kupunguza au kuzuia:

- > tishio kubwa la maisha
- > unyanyasaji wa mtoto
- > unyanyasaji wa nyumbani na familia au
- > kulinda masilahi yako au/na usalama wa wengine.

Kutumia habari ili kuboresha huduma za afya

SA Health inaweza kutumia taarifa kuhusu huduma ya afya yako ili kuboresha huduma za afya, kupanga kwa ajili ya huduma za baadaye, au kwa ajili ya utafiti. Kama hii ikitokea, habari zitakazotumika hazitajumuisha taarifa zozote za kibinagsi ambazo zinaweza kukutambulisha wewe.

Kama unaamini kwamba taarifa yako binagsi zimeshirikishwa bila sababu u kupatikana, unaweza kujadili na huduma za afya au kufanya malalamiko kwa Kamishna wa Malalamiko (tazama ukurasa 24 kwa maelezo ya mawasiliano) au kwa Kamati ya Siri ya Australia ya Kusini.

Kamati ya Usiri inaweza kupigwa simu kwa 08 8204 8786 or
www.archives.sa.gov.au.

Upatikanaji wowote wa makusudi yasiyofaa ya kumbukumbu ya afya unachukuliwa kwa umakini sana. Kama hii ikitokea utaweza kupewa taarifa.

8. Maoni – haki ya kutoa maoni na/au malalamiko

SA Health inatia moyo wagonjwa/wateja, familia, walezi na jamii kwa sisi na kutoa maoni. Maoni, pongezi, malalamiko na mapendekezo hutusaidia kuboresha huduma zetu za afya.

Una haki ya:

- > kutoa maoni na kuuliza maswali kuhusu huduma ya afya yako na uzoefu
- > kutujulisha kama unadhani huduma ya afya yako haiendi kama ilivyopangwa
- > wasiwasi zako au malalamiko yanashughulikiwa vizuri na mara moja kutolewa mælezo na kuomba msamaha
- > kutupatia maoni yako.

Jinsi ya kutoa maoni kwa huduma za afya:

- > kueleza matatizo yako kwa kuzungumza na mfanyakazi anayekuangalia katika huduma ya afya. Unaweza pia kupiga simu au kuandika kwa huduma za afya.
- > kama wewe unajisikia kuwa wasiwasi zako hajijatatuliwa, unaweza kuwasiliana na Mshauri wa Watumiaji / Mgonjwa, Mratibu wa Maoni ya Mgonjwa au Mratibu wa Ubora (katika mæneo ya Vijijini). Tembelea www.sahealth.sa.gov.au/yourrightsandresponsibilities.

Tunachukua matukio yote na taarifa zinazokaribia kupotea kwa makini. Tunavitumia kujifunza namna ya kuboresha huduma na kuepuka matukio kama hayo katika siku zijazo. Tukio lolote unalohusika litaimamiwa kwa njia ya wazi na muonekano

Kama wewe hauna furaha na majibu kwa maoni yako unaweza kuwasiliana na mashirika ya malalamiko huru ya utetezi. Mashirika haya ni pamoja na:

Kamishna wa Malalamiko wa Afya na Huduma za Jamii

Ofisi huru ambayo inasaidia watu (watumia huduma, watunzaji na watoa huduma) na malalamiko kuhusu huduma za afya au jamii katika Australia ya Kusini.

Jumatatu hadi Ijumaa saas 3.00 asubuhi hadi saa
11.00 jioni (9.00am - 5.00pm)

Simu 08 8226 8666 au vijijini piga bure 1800 232 007

www.hcsc.sa.gov.au

Mpango wa Kutembelea Jamii wa Ulemavu na Afya ya Akili

Shirika huru la malalamiko ambalo hukagua vituo vilivyopitishwa kwa matibabu na kutetea haki za watu wenye ulemavu na wagonjwa wa afya ya akili ndani ya vituo vyatubabu.

Simu: 08 7425 7802 au Kupiga bure vijijini 1800 606 302 www.sa.gov.au/ (harafu tafuta Community Visitor Scheme).

Ofisi ya Wakili wa Umma

Shirika la kujitegemea ambalo linashauri, kupitisha na kutetea watu wenye uwezo mdogo wa kufanya maamuzi, na husaidia kutatua migogoro kuhusu maamuzi ya afya

Simu: 08 8342 8200 au kupiga vijijini bure 1800 066 969

www.opa.sa.gov.au

Rufaa

Una haki ya kutafuta usuluhishi kuitia Ofisi ya Wakili wa Umma kama kuna tatizo kuhusu Mwelekeo wa Afya wa Juu au utoaji au kukataa kwa matibabu au huduma za afya.

Kwa habari za haraka baada yamasaa ya kazi kwa kuwasiliana na Ofisi ya Wakili Jamii piga kwenye simu:
(08) 8378 3333.

Una haki ya kukata rufaa kwa Utawala wa Mahakama ya Australia ya Kusini ya Jamii (SACAT) (zamani Bodi ya Ulezzi), kama wewe uko kwenye sheria ya Afya ya Akili ya 2009 au sheria ya matibabu ya ndani ya kifungu cha 32 amri chini ya Ulezzi na Utawala ya 1993 na haujaridhika na utaratibu

Una haki ya kukata rufaa juu ya uamuzi wa SACAT katika Mahakama ya Wilaya au Mahakama ya Ulezzi na Sheria ya Tawala za 1993.

SACAT inaweza kupigiwa simu 1800 723 767 or www.sacat.sa.gov.au.

Haki na Majukumu yako yanaunda Mkataba wa Wagonjwa 'Hospitali, kama inavyoolezwa chini ya Mkataba wa Taifa wa Matunzo ya Afya kati ya Australia ya Kusini na Serikali ya Jumuiya ya Madola Serikali.

Nakala zaidi ya kijitabu hiki inaweza kupatikana kutoka:

Kwa wagojwa na Walezi:

www.sahealth.sa.gov.au

Kwa Hospitali na Huduma za Afya:

SA Health Distribution Centre

Barua pepe: healthPSCMSOCustomerService@sa.gov.au

Faksi: 08 8124 4655

www.sahealth.sa.gov.au

Public-I1-A1



Waraka umerudiwa upya na kupitishwa
na SQCAG * kwa ajili ya watumiaji na
jamii Februari 2016.



www.ausgoal.gov.au/creative-commons

© Idara ya Afya na Uzee, Serikali ya Australia ya Kusini.

Haki zote zimehifadhiwa. ISBN: 978 07 03 898 276 FIS: 16002.1 April 2016

*Kundi la Ushauri wa Usalama wa SA Health Usalama na Jamii..



Government
of South Australia

SA Health